**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

# *Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji kwa Waandishi wa Habari kuhusu Hatua Iliyofikiwa katika Maandalizi ya Utekelezaji wa Dira 2050*

***Dar es Salaam, Jumatano, 24 Septemba 2025***

---

1. Serikali ilizindua rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo (Dira 2050) tarehe 17 Julai 2025, Jijini Dodoma.
2. Kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2050, Serikali ilishakamilisha maandalizi ya Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Maendeleo (Long-Term Perspective Plan – LTPP). Mpango huu utatekelezwa kupitia mipango ya muda mfupi ya miaka mitano (Five Year Development Plans- FYDPs).
3. Kufuatia kuzinduliwa rasmi kwa Dira 2050, na kukamilika kwa maandalizi ya LTPP, Serikali iliunda Timu ya Wataalam ya kuandaa Mpango wa nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Fourth Five Year Development Plan – FYDP4). Timu hii inajumuisha wajumbe 22 kutoka sekta ya umma na sekta binafsi, ikiongozwa na Dkt. John Mduma.
4. Pamoja na mambo mengine, Timu ya Wataalam itabainisha na kupendekeza programu na miradi ya kielelezo (flagship projects) na miradi ya kimkakati (strategic projects) itakayotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano, kuanzia Julai 1, 2025.
5. Katika hatua ya awali, Timu ya Wataalam imebaini na kupendekeza miradi 12 (kati ya miradi 17) ya kielelezo inayoendelea kutekelezwa kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

2021/22 – 2025/26 iingizwe na kutekelezwa katika FYDP 4. Miradi mitatu imeshakimilika. Miradi hii ni:

i) Mradi wa kufua umeme wa maji wa Bwawa la Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydropower Project – JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115
ii) Mradi wa ujenzi wa madaraja makubwa na madaraja ya juu (flyovers) 13
iii) Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Mkulazi

6. Miradi ya kielelezo kutoka FYDP 3 inayopendekezwa kuendelea kutekelezwa kama sehemu ya utekelezaji wa FYDP 4 ni pamoja:

*i) Mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa SGR wenye vipande (lots) nane*
*ii) Mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lenye urefu wa KM 1443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), ambao umefikia asilimia 55*
*iii) Ununuzi wa meli na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko, ambao umefikia asilimia 75*
*iv) Mradi wa kufufua umeme wa Ruhidji (MW 358), ambao umefikia asilimia sita*
*v) Mradi wa kufua umeme wa Rumakali (MW 222), ambao umefikia asilimia saba*
*vi) Mradi wa ujenzi wa Gesi (LNG) Lindi, ambao umefikia asilimia sita*
*vii) Mradi wa utafutaji wa mafuta na gesi katika Kitalu cha Eyasi-Wembere, Manyara, ambao umefikia asilimia tano*
*viii) Mradi wa utafutaji wa mafuta na gesi Mnazi Bay-Mtwara, ambao umefikia asilimia sita*
*ix) Mradi wa Magadi soda ya Engaruka-Arusha, ambao umefikia asilimia tano*
*x) Mradi wa Kuendeleza Kanda Maalum ya Kiuchumi wa Bagamoyo (Bagamoyo Eco Maritime City), ambao umefikia asilimia tano*
*xi) Ujenzi wa reli ya kusini kwa kiwango cha kimataifa kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay na matawi ya Liganga na Mchuchuma, ambao upo katika hatua za awali za maandalizi*
xii) *Mradi wa makaa ya Makaa Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga, ambao umefikia asilimia sita*.

7. Kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga
    i) Mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na chuma Liganga ni muhimu katika utekelezaji wa ajenda ya kitaifa wa ujenzi wa viwanda kama moja ya sekta za kimageuzi zilizobainishwa katika Dira 2050. Makaa ya mawe yana fursa ya kuzalisha umeme kwa ajili ya viwanda, wakati chuma kinatarajiwa kutoa malighafi muhimu kwa ajili ya viwanda na sekta ya ujenzi kwa ujumla. Utekelezaji wa mradi wa kuzalisha na kufua chuma Liganga utaifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa nne wa chuma katika bara la Afrika, baada ya Afrika Kusini, Misri na Libya.
    ii) Uamuzi wa kutekeleza mradi huu ulifanywa na Baraza la Mawaziri mwaka 1996. Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) ilikabidhiwa jukumu la kutekeleza mradi huu kwa kushirikiana na sekta binafsi. Uamuzi huu ulihuishwa na Baraza la Mawaziri mwaka 2007 ambapo NDC ilielekezwa kutafuta wawekezaji wa kutekeleza mradi huu kwa njia ya ushindani. Jumla ya makampuni 48 yalijitokeza kuomba kuwekeza katika mradi.
    iii) Kampuni iitwayo Sichuan Hongda Corporation (SHG) Ltd. kutoka China ilishinda na wakaingia mkataba na NDC Tarehe 21 Septemba 2011. Kama sehemu ya utekelezaji wa mkataba, NDC na SHG walianzisha kampuni ya ubia iliyoitwa Tanzania *China International Mineral Resources Limited (TCIMRL*), ambapo NDC ilikuwa inamiliki asilimia 20 na SHG ikimiliki asilimia 80.
    iv) Tarehe 30 Juni 2014 kupitia kilichokuwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) ilisaini mkataba wa utendaji na Kampuni ya TCIMRL, wenye kuzingatia, pamoja na mambo mengine, vivutio mbalimbali.
    v) Mwaka 2015 utekelezaji wa mradi ulisitishwa baada ya Serikali kubaini kuwa baadhi ya masharti ya mkataba wa ubia (kati ya NDC na SHG) hayakuzingatia kikamilifu maslahi mapana ya nchi.
    vi) Katika kukwamua mradi huu, mwaka 2017 Serikali iliunda Timu Maalum ya Majadiliano (Special Presidential Government Negotiation Team) kwa lengo la kupitia upya mikataba ya mradi huu na kuondoa vipengele vilivyoonekana vina changamoto. Hata hivyo, hadi 2020 hapakuwa na mwafaka kati ya Serikali na mwekezaji.

vii) Mwaka 2024 Kampuni ya SHG ilinunuliwa na Kampuni ya *Shudao Investment Group Company Ltd. (SDIG*) inayomilikiwa na Serikali ya Jimbo la Sichuan.

viii) Tangu mwezi Januari 2025 Serikali imekuwa ikijadiliana na Kampuni ya SDIG kuhusu vipengele vya mkataba ambavyo Serikali haikuridhika navyo. Mazungumzo yapo hatua za mwisho na tumeshakubaliana mambo mengi ya msingi.

ix) Serikali imeshalipa fidia katika eneo la mradi na sasa linamilikiwa na Serikali.

8. Aidha, kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2050 na FYDP 4, Serikali inaendelea na mapitio ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI). Mpango huu unalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekazaji wa ndani na nje.

9. Utekelezaji wa Dira 2050 unategemea ushiriki wa sekta binafsi. Serikali imejipanga kuendelea kuchochea ukuaji wa sekta binafsi nchini kwa kuijengea uwezo wa kimtaji na kimaarifa ili iweze kuchukua nafasi yake katika uwekezaji na kufanya biashara na kuwa na uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa. Katika utekelezaji wa Dira 2050, Serikali itaweka maalum ya kuchochea ukuaji wa biashara ndogo na za kati za watanzania. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kuvutia wawekezaji kutoka pembe zote za dunia.

Imetolewa na

Kitila Alexander Mkumbo

**WAZIRI WA NCHI**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

Dar es Salaam, Jumatano 24 Septemba 2025.